Maelekezo ya Mafunzo Kwa Sala ya Uinjilisti

KIMEANDIKWA NA
EVELYN CHRISTENSON

KIMETOLEWA KWA MATUMIZI YA
USHIRIKA WA KIMATAIFA WA WANAWAKE
WA MWAKA 2000

Inside front cover

EVELYN AKUKARIBISHA

Ninayo furaha kwamba umeamua kujiunga nami katika kuwafikishia wapotevu neno la Yesu kwa kukitumia kitabu hiki.

Hamu kubwa ya moyo wangu ni kwamba mataifa yote yajazwe kwa vikundi vya wakristo watatu watatu - wakieneza upendo, wakijali masilahi ya wengine, wakitoa ushuhuda, hadi ulimwengu wote ujae waumini wapya katika Yesu.

Kitabu hiki kina kiini cha yale ambayo Mungu amenifundisha maishani mwangu, na nimemshuhudia akitenda makubwa na maajabu, nilivyokuwa nikifundisha mwenyewe, neno takatifu kwa maelfu na maelfu.

Hiki ndicho kiini cha injili ya Yesu ambayo imefupishwa katika kurasa hizi chache. Kitabu hiki kimeandikwa katika lugha rahisi makusudi ili kila mtu ulimwenguni akifahamu, huku kikiwa na undani wa kutosha kushirikisha yote yaliyo muhimu katika Biblia na kiweze kuufikia ulimwengu mzima kwa niaba ya Yesu.

Kimeandikwa kwa ufupi, na si ghali, ili wote ulimwenguni waweze kukinunua.

Kimeandikwa katika maelezo mafupi kwa nia ya kutoa kwa udhahiri mambo muhimu ambayo yangalipotea kama yangaliandikwa katika mitindo mingine. Pia kwa kukiandika katika mtindo huu, kimeweza kuhusisha katika kurasa chache hizi, yote utakayoyahitaji ili kuwafikia wote walioko karibu nawe, na wale ambao hawajafikiwa, kwa niaba ya Yesu.

Kitafaa pia hata ikiwa utakisoma ukiwa peke yako, na wenzako wachache, au kukifunza darasani. Kisha ukiyafuata mafundisho yake ya Biblia hatua kwa hatua, utapata furaha isiyoelezeka ya kushuhudia uwezo wa Mungu ukiwafikia wale ambao umewaombea wakiwa na maisha mapya katika Yesu Kristo.

Uwe na uhakika kwamba nitakuwa nikikuombea unaposoma na kuwafikia, pamoja nami, wale wapotevu, kwa niaba ya Yesu.

Nitatumaini kwamba umeanza kuunda kikundi chako cha watu watatu sasa. Wasiliana nami jinsi Mungu anavyokitumia kitabu hiki.

Evelyne Christenson, Mmoja wa wenyeviti,
Ushirika wa Wanawake wa Amerika kaskazini wa mwaka 2000

MAELEZO YA MCHAPISHAJI

Evelyne hakutaka maelezo haya yachapishwe; lakini sisi, wachapishaji, twaonelea ni muhimu kwako kuyajua.

Wengi wenu kote ulimwenguni walijulishwa kwa Evelyne Christenson kupitia kitabu mashuhuri kiitwacho *'kinapotendeka wanawake wanaposali'* kilichobarikiwa na Mungu, na ambacho ni kiini cha kujitolea katika sala maishani mwa maelfu ya wanawake, wanaume, makasisi na makanisa. Pia labda umesoma kimoja kati ya vitabu vitano ambavyo ameviandika vilivyofuata, viwili kati yavyo ambavyo vimeshinda tuzo mashuhuri la Gold/Platinum; au labda umehudhuria mojawapo ya warsha ambazo ameziandaa katika kila bara. Ametoa ukarimu na upendo wake bila malipo, hata wakati anapotoa mapato yanayotokana na mauzo ya kitabu hiki sasa kuendeleza ushirika wa sala wa mwaka 2000 ulimwenguni.

Ndiye mwanzilishi na mwenyekiti wa halmashauri ya umoja wa ushirika wa sala, ambao miongoni mwa shughuli nyingine, hudhamini radioni, vipindi, vya sala zake kila juma katika nchi nyingi. Kurasa nyingi zingelihitajika kuorodhesha matuzo ya heshima ambazo ametuzwa. Hata hivyo angezipuuza zote.

Maelfu ya maili ambayo amesafiri, na saa nyingi ambazo amesimama akifundisha, ni sehemu ya sala aliyosali zaidi ya miaka thelathini iliyopita. "Baba uuwezeshe ulimwengu mzima upate uwezo katika sala, ambao umetupatia kupitia Roho Mtakatifu ili kuwaondoa wapotevu kutoka ufalme wa shetani na kuwaleta katika ufalme wa Mwana wako mpendwa. Oh, Baba nataka kuufikia ulimwengu mzima kipitia sala.

Unashika mkononi mwako jibu la Mungu ukiikubali sala ya Evelyne Christenson.

YALIYOMO

Evelyne akukaribisha	Sehemu ya ndani ya jalada la mbele
Jinsi ya kukitumia kitabu hiki	2
SEHEMU YA KWANZA — Kwa nini kitabu hiki ni muhimu	3
SEHEMU YA 2 — Matayarisho yetu binafsi	7
SEHEMU YA 3 — Uwezo wa Mungu wa kuenea ulimwenguni	14
SEHEMU YA 4 — Jinsi ya kuwaombea wapotevu	18
SEHEMU YA 5 — Kuombeana	24
SEHEMU YA 6 — Jinsi ya kuwafikia kwa niaba ya Yesu	27
Kutoka viongozi wa kimataifa	31
Fomu ya kikundi cha watu watatu	31
Jinsi ya kukiagiza kitabu hiki	Sehemu ya ndani ya jalada la nyuma

Haki ya nakili 1992 Evelyne Christenson.

Kimetolewa kutumiwa na ushirika wa maombi ya wanawake wa mwaka 2000

Kitabu hiki hakipasi kubadilishwa, au kunukuliwa katika Amerika kaskazini bila idhini iliyoandikwa na mwandishi wake. Chaweza kutafsiriwa na kuchapishwa katika lugha nyingine, idhini ikitolewa na ushirika wa kimataifa wa wanawake wa mwaka 2000.

Maandishi yote matakatifu yametolewa katika New American Bible (ruhusa ya kuyatumia imetolewa) isipokuwa pale imeelezwa.

Kimechapishwa nchini Amerika
na
THE CONGER PRINTING COMPANY INC.
ATLANTA GEORGIA 30318

JINSI YA KUKITUMIA KITABU HIKI

Twaamini kwamba Mungu ametoa njozi ya uwezo wake ambayo yaweza kufanya kazi wakati sala za kikundi cha watu watatu zinapoenea na kuwa ushirika wa ulimwengu wote.

Madhumuni ya kitabu hiki ni kuwafikia wanawake katika kila taifa, kusali katika vikundi vya watu watatu, hasa kwa jamaa na rafiki ili wazaliwe upya, waokoke katika ufalme wa Mungu. Na pili, kwamba watu wa Mungu watawaombea wale ambao hawajafikiwa na neno la Mungu ulimwenguni ili waisikie injili ya Yesu Kristo.

Hamu, nia, wazo na uandishi wa kitabu hiki ziliongozwa na Roho Mtakatifu. Kitabu hiki ni cha ulimwengu wote katika misingi yake ya kiinjili. Ni rahisi, lakini kina maana sana hivi kwamba kukitumia katika sala zako kutazua majibu ya Mungu yenye uwezo mkubwa.

KITABU HIKI CHAWEZA KUTUMIWA KATIKA NJIA TATU:

Kwanza, waweza kuunda kikundi cha sala cha watu watatu, na rafiki wengine au jamaa zako kujifunza na kukitumia kitabu hiki kwa pamoja. Kisha kila mtu katika kikundi atawachagua watu watatu ambao hawajaokoka ambao nyote mtawaombea. Kisha kikundi chenu kitachagua kundi la watu ambao hawajasikia kumhusu Yesu. Jaza kadi ya kikundi chako na maombi, kisha nyote watatu muwe mkikutana kila juma na kuwaombea watu wenu tisa ambao hawajaokoka, na nchi yako (tazama maelezo kamili katika sehemu ya 4 ya kitabu hiki.) Pili , makanisa, madhehebu, mashirika ya kikanisa na miji yaweza kutayarisha msisimko wa kiinjili kupitia kutayarisha na kufunza sala za vikundi vya watu watatu. Ikiwezekana ni muhimu kuwa na wakati maalum wa kuwahimiza, kuwafundisha na kuwasajili watu katika vikundi vya watatu. Vikundi hivi vinapoundwa, vinasimamiwa na kiongozi wa mpango katika shirika hilo. Mikutano ya hadhara ya maombi ya mara kwa mara ya vikundi vyote pamoja ya kuvihimiza, kumsifu Mungu, kuelezana, kupata mafunzo zaidi, na kusali pamoja, yafaa iwe ikifanywa mara kwa mara. Wanaookoka kutokana na maombi ya vikundi yafaa, ikiwezekana, wafuatiliwe mara moja na kushirikishwa kanisani au katika shirika. Tatu, ikiwa humjui yeyote unayeweza kuunda kikundi naye, sali hadi Mungu atakapokuonyesha watu hao, au kuwaleta kwako.

KUFUNDISHA KITABU HIKI

Kumbuka kwamba baada ya kujifunza na kutumia yaliyomo katika maisha yako,waweza kuwa mwalimu na mtayarishi wa vikundi zaidi vya maombi miongoni mwa marafiki, kanisa au shirika lako. Kisha waweza kuwahimiza kufanya vivyo hivyo. Kitabu hiki kiliandikwa katika lugha rahisi, na kwa ufupi ili wakristo waliyo na nia ya kuwaombea wapotevu wasikitumie tu wao binafsi, bali waeneze zaidi matumizi yake.

UNAPOFUNDISHA:

* Hakikisha kwamba unasali unapokitumia kitabu hiki,
* Kitumie wewe mwenyewe kabla ya kuwatarajia wengine kuyafuata mafunzo yako.
* Tumia maelezo kutoka maishani mwako, inapowezekana.
* Biblia ndiyo mwamuzi wa mwisho, wala sivyo wanavyofikiri watu wengine.
* Viongoze vikundi vyote darasani mwako kulingana na maagizo.
* Waombeeni wanafunzi wako kila siku, na uwatake nao wakuombee pia.

Kitabu hiki hakikukufikia kibahati. Mungu amekuchagua ujifunze kwa makini na uutie katika sala zako ukweli wa Biblia. Mungu amekufichulia kuhusu sala iliyojibiwa. Wewe ni mteule wa Mungu wakati huu. Tunakuombea.